

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA



**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO YA ASILIMIA KUMI INAYOTOLEWA
KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 8 (1))

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anatangaza uwepo wa Fedha kwa ajili ya kuvikopesha Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu, ambapo jumla ya **Shilingi 4,500,000,000/=** zimetengwa katika robo ya Pili ya mwaka wa fedha **2024/2025**. Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi ya Mikopo katika Ofisi za Kata zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- (i) Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri kupitia Mfumo wa **“Wezesha Portal”**;
- (ii) Kikundi kiwe kinajishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali;
- (iii) Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake;

- (iv) Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali;
- (v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea; na
- (vi) Kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo;-

1. Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Mtaa;
2. Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo;
3. Andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo; na
4. Taarifa ya akaunti ya benki (Bank Statement).

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielekroniki wa "**Wezesha Portal**" kupitia tuvuti ya (***mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz***).

NB;

- ❖ *Vikundi Vyote vilivyotuma awali Maombi yao ya Mkopo kupitia Mfumo wa "Wezesha Portal", Maombi yote yamefutwa hivyo, wanapaswa Kuomba upyaa kwa kufuata utaratibu wa sasa; na*
- ❖ *Vikundi vyote Vitakavyoomba Mkopo wawasiliane na Afisa Maendeleo wa Kata kwaajili ya kuwapa maelekezo juu ya Andiko la Mradi.*

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **22 mwezi 11 mwaka 2024.**

Tangazo hili limetolewa Leo Tarehe 21/10/2024 na;
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma.


.....
Dr. Frederick D. Sagamiko

**MKURUGENZI WA JIJI
DODOMA**

